

LINDI WOMEN PARALEGAL AID CENTRE - LIWOPAC



SATF
social action trust fund



TAARIFA YA MWAKA 2020



Imeandaliwa na:

LIWOPAC, Desemba 2020.

UJUMBE WA MWENYEKITI WA BODI YA SHIRIKA

Kwa niaba ya Bodi ya wakurugenzi wa shirika la LIWOPAC, naandika ujumbe huu kwa madhumuni ya kutoa shukrani zangu za dhati kwa utekelezaji wa shughuli za shirika kuanzia Januari hadi Desemba 2020. Nimekuwa nikihusishwa kuanzia mwanzo wa utekelezaji wa shughuli hadi mwisho wa shughuli hizi zilizofanyika na nilitumia muda wangu mwingi katika kuhakikisha haki za msingi za wanawake na watoto zinalindwa na kuzingatiwa kwa mustakabali wa jamii ya Lindi na Tanzania kwa ujumla.

LIWOPAC imedhamiria kutanua wigo wa utoaji huduma za msaada wa kisheria katika jamii. Ni Imani yetu kubwa kuwa watoa huduma ya msaada wa kisheria ambao ndio nyenzo muhimu katika shirika wameimarika na kufanya kazi kwa kuzingatia sheria na taratibu zilizopo katika tasnia ya Asasi za kiraia pamoja msaada wa kisheria. Sambamba na hilo pia uhamasishaji kuhusu usawa wa kijinsia umetolewa kwa wananchi na jamii kwa ujumla kupitia kwa mabalozi wa kupinga vitendo vya ukatili wa kijinsia. Ni matarajio yetu kuwa jitihada kubwa zilizofanywa kwa mwaka huu 2020 zimeleta matunda makubwa ya mahitaji ya kudai haki kwa kundi kubwa la jamii.

Katika kuwasilisha taarifa hii, tunajiona wenye bahati kubwa ya kuimarisha uendeleu wa miradi iliyopo katika maeneo ya utekelezaji. Timu ya utekelezaji wa miradi itaendelea kuwa karibu na kutembelea mara kwa mara vituo vya msaada wa kisheria vilivyopo kila wilaya, mabalozi wa kupinga ukatili wa kijinsia katika ngazi ya vijiji na wanafunzi waishio katika mazingira magumu ili kundeleza upatikani wa huduma kwa wanufaika wote.

Ahsante, Nawatakia usomaji mzuri wa taarifa hii.

AFWILE MBEMBELA

.....

MWENYEKITI WA BODI-LIWOPAC

LINDI WOMEN PARALEGAL
AID CENTRE
(LIWOPAC)
P. O. Box 408, LINDI

NENO LA SHUKRANI

LIWOPAC inatoa shukrani kwa wahisani na wadau wote ambao wamechangia kwa kiasi kikubwa katika ukamilishwaji wa taarifa hii ya utekelezaji wa shughuli kwa mwaka 2020 na kufanikisha malengo ya shirika. Shukrani zetu za dhati zinaenda kwa Legal Services Facility (LSF), OXFAM Tanzania na SATF ambao wamewezesha msaada wa kifedha na kitaalamu katika kipindi chote cha utekelezaji wa shughuli zetu.

Tunapenda kutoa shukrani zetu za dhati kwa kazi kubwa na nzuri iliyofanywa na watoa huduma za msaada wa kisheria, mabalozi wa kupinga vitendo vya ukatili wa kijinsia, vituo vya msaada wa kisheria vilivyopo kila wilaya katika mikoa ya Lindi na Mtwara kwa kujitua muda wote kufanikisha utekelezaji wa shughuli za miradi. Tunapenda kuwashukuru kwa kupenda kufanya kazi muda wote ili kuisaidia jamii ya mikoa ya Lindi na Mtwara na Tanzania kwa ujumla.


Sambamba na hilo, LIWOPAC tunatuma salamu zetu za shukrani kwa viongozi wote wa Serikali katika Halmashauri za mikoa ya Lindi na Mtwara kwa utendaji kazi na huduma zilizotukuka katika kipindi chote cha utekelezaji wa shughuli za shirika. Shukrani za kipekee ziende kwa Mkuu wa mkoa wa Mtwara, Mkuu wa mkoa wa Lindi, Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa ya Lindi na dawati la jinsia la polisi wilaya na mkoa wa Lindi kwa ushirikiano mkubwa walioutoa kwa watoa huduma za msaada wa kisheria na mabalozi wa kupinga vitendo vya ukatili wa kijinsia, ili kuhakikisha rasilimali zilizowekwa zinatumiwa ipasavyo na kwa uwazi mkubwa katika kuiletea jamii tunda la haki.

Mwisho lakini sio kwa umuhimu, LIWOPAC inapenda kutoa shukrani kwa wanufaika wote wa mradi na watoa huduma kwa ujumla ambao mara kwa mara walikua wakitembelea na kufanya mahojiano ili kutathmini maendeleo ya miradi. Juhudi zao za moja kwa moja zimeleta matokeo chanya ambayo yamesaidia shirika katika uwajibikaji, kukabiliana na changamoto mpya na kuwezesha utoaji bora wa huduma za kisheria katika mikoa ya Lindi na Mtwara.

COSMA BULU


.....

MKURUGENZI-LIWOPAC



YALIYOMO:	
UJUMBE KUTOKA KWA MWENYEKITI WA BODI YA SHIRIKA	2
NENO LA SHUKRANI	3
RAMANI IKIONESHA WILAYA ZA MIKOA YA LINDI NA MTWARA.	5
MUHTASARI WA TAARIFA	Error! Bookmark not defined.
1.0 UTANGULIZI.....	7
1.1 HISTORIA YA SHIRIKA.....	7
1.2 DIRA:.....	8
1.3 DHIMA:.....	8
2.0 USHIRIKI WA WADAU	8
3.0 MATOKEO YALIYOPATIKANA KATIKA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI.	9
3.1 Tokeo na.1: Huduma bora za msaada wa kisheria zinaendelezwa katika jamii husika hadi mwaka 2020.....	9
3.1.1 Mafanikio.....	9
3.2 Tokeo na.2 Kuongeza uelewa wa sheria kwa jamii ya Lindi na Mtwara kufikia mwaka 2020.	9
3.2.1 Mafanikio:.....	9
3.2.2 Mchanganuo wa idadi ya watu waliofikiwa na mradi wa LSF 2019/2020	10
3.3 Tokeo na.3: Kuongezeka kwa uelewa wa Haki za kijinsia katika maeneo ya utekelezaji.....	10
3.3.1 MAFANIKIO.....	10
3.3.2: Kuongezeka kwa mabadiliko ya mitazamo na mienendo chanya katika jamii.	10
3.3.3: Serikali za mitaa kuwa na uwezo wa kuzitafsiri na kuzifanyia kazi sera na sheria zinazohusu usawa wa kijinsia katika jamii husika.	11
3.3.4: Kuongezeka kwa utoaji huduma bora na salama kwa wahanga wa matukio ya ukatili wa kijinsia.....	11
3.3.5: Kuongezeka kwa huduma zinazokidhi changamoto za wanawake waishio katika mazingira magumu katika jamii.	12
3.3.6: Kuboresha uwezo wa kufanya tafiti katika maeneo ya kimradi ya shirika. ..	Error! Bookmark not defined.
3.3.7: Kuongeza nafasi za wanawake katika uongozi.....	12
3.4 Tokeo na 4: Kuimarika kwa kulindwa haki za mtoto	13
3.4.1 MAFANIKIO.....	13
3.5 Tokeo na. 5: Utafiti katika masuala yanayohusiana na utekelezaji wa programu za LIWOPAC	13
3.5.1 Mafanikio:	13
4.0: MAFUNZO, CHANGAMOTO NA MAPENDEKEZO.....	14
4.1 MAFUNZO.....	14
4.2 CHANGAMOTO	15
4.3 MAPENDEKEZO	15
5.0. HITIMISHO NA VIAMBATANISHO	16

WILAYA ZA MKOA WA LINDI - TANZANIA



Ramani ikionesha wilaya za mikoa ya Lindi na Mtwara.

MUHTASARI WA TAARIFA

Taarifa hii ya mwaka 2020 imetokana na shughuli zilizotekelezwa na Shirika la msaada wa kisheria kwa wanawake na watoto katika mikoa ya Lindi na Mtwara. Taarifa hii imefafanua zaidi kuhusu upatikanaji wa haki, usawa wa kijinsia na programu ya kuwasaidia wanafunzi waishio katika mazingira magumu. Shughuli hizi zimefanywa na LIWOPAC kulingana na ukubwa wa tatizo, rasilimali zilizopo, jiografia ya maeneo na changamoto katika maeneo ya kufanyia kazi. Pia taarifa hii imetumia namba pamoja na maandiko katika kuelezea jitihada za shirika na matokeo yaliyofikiwa.

Taarifa hii imegawanyika katika vipengele vitano (5) ambavyo ni; 1. Utangulizi 2. Ushiriki wa wadau 3. Matokeo ya shughuli za miradi 4. Mafunzo, Changamoto na Mapendekezo 5. Hitimisho na Viambatanisho. Utangulizi unampa msomaji wa taarifa hii uwanja wa kufahamu kwa ufupi yaliyomo katika taarifa hii ikiwemo na jiografia ya shughuli zilizofanywa na miradi. Sehemu ya ushiriki wa wadau inaeleza kwa kina ni wadau gani shirika wameshirikiana nao katika utekelezaji wa shughuli za miradi. Sehemu ya matokeo ya shughuli za miradi inampa msomaji wa taarifa hii kujua kuhusu utekelezaji wa miradi pamoja na matokeo yaliyopatikana. Pia mbinu na rasilimali ambazo zimetumika, uchambuzi na majadiliano katika kutafsiri mafanikio ya shughuli zilizofanyika, sambamba na hayo sehemu inatoa fursa ya kuonesha kwa ujumla mafanikio yaliyofikiwa kupitia miradi iliyotekelezwa.

Sehemu ya mafunzo inaonesha mambo ambayo yamepatikana kutokana na utekelezaji wa shughuli, pia changamoto zilizojitokeza na Mapendekezo ya utatuzi wa changamoto zilizoainishwa ili kuwawezesha wadau wa maendeleo kuboresha mipango kazi ya baadaye katika kuhakikisha jamii yenye haki na usawa inapatikana katika mikoa ya Lindi, Mtwara na Tanzania kwa ujumla. Hitimisho linakamilisha taarifa kwa kukazia mambo yote yaliyoelezewa ndani ya taarifa. Mwisho ni viambatanisho ambavyo ni Mpango kazi wa Mwaka 2021, Taarifa ya mahesabu ya mwaka yaliyokaguliwa na hadithi za mafanikio.

1.0 UTANGULIZI

Hii ni taarifa ya utekelezaji wa shughuli za shirika kwa mwaka 2020 kuanzia mwezi Januari hadi Desemba. Taarifa hii imeakisi shughuli zote zilizofanywa na shirika katika kipindi cha mwaka mzima. Taarifa hii imeandaliwa kutokana na matokeo yaliyopatikana katika ufuatiliaji na tathimini maeneo ya mradi, taarifa za mwezi na robo mwaka zinazoletwa na mabalizi wa kupinga ukatili wa kijinsia na wasaidizi wa kisheria, Matokeo ya tathimini ya mwisho wa mradi na habari za mafanikio zilizopatikana wakati wa kutembelea wanufaika wa mradi.

Taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu 5. **Sehemu ya 1: Utangulizi na Historia ya shirika, Sehemu ya 2: Ushiriki wa wadau, Sehemu ya 3: Matokeo ya shughuli za Miradi mbalimbali, Sehemu ya 4: Mafunzo, Changamoto na Mapendekezo, Sehemu ya 5: Hitimisho na Viambatanisho ambavyo ni Mpango kazi wa Mwaka, Habari za Mafanikio na Taarifa ya mahesabu ya mwaka yaliyokaguliwa.**

1.1 HISTORIA YA SHIRIKA

LINDI WOMEN PARALEGAL AID CENTRE (LIWOPAC) ni shirika lisilo la kiserikali linalotoa huduma ya msaada wa kisheria kwa wanawake, watoto na jamii kwa ujumla katika mkoa wa Lindi Mtwara. Ni shirika lisilotengeneza faida binafsi na linatoa huduma zake pasipo na malipo yoyote kwa jamii inayohitaji huduma za msaada wa kisheria. Shirika lilianzishwa mwaka 2001 kufuatia ushawishi kutoka kwa shirika la Women Legal Aid Centre (WLAC) na kupata usajili NO. 11989 mwaka 2003 chini ya sheria kifungu namba 337 ya mwaka 1954. Aidha mwaka 2008 LIWOPAC ilipata cheti cha ukubalifu chenye NO. 0760, hii ni kuthibitisha kuwa shirika linafanya shughuli zake kihalali na linatambulika na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa sasa shirika linafanya kazi Tanzania Bara na limefanikiwa kutoa huduma zake kwa Halmashauri za wilaya zote za mkoa wa Lindi na Mtwara ambazo ni Nachingwea, Ruangwa, Lindi Manispaa, Mtama, Kilwa, Liwale, Mtwara Manispaa, Mtwara vijijini, Masasi, Nanyumbu, Newala na Tandahimba. Tangu kuanzishwa kwake, Shirika limefanya kazi na wadau mbalimbali wa maendeleo na wafadhili ambao wanatoa ruzuku zinazoweza utekelezaji wa shughuli zake. Wadau hao ni kama vile Legal Services Facility (LSF), PACT, Concern World Wide, Foundation for Civil Society (FCS), RFE and PILPIG na Oxfam Tanzania.

1.2 DIRA:

LIWOPAC inaiona jamii inayoheshimu na kulinda haki za msingi za wanawake na watoto mkoani Lindi.

1.3 DHIMA:

LIWOPAC ipo kwa ajili ya kujenga uwezo kwa wanawake na watoto Mkoani Lindi kwa njia ya kutoa msaada wa kisheria, mafunzo na utetezi kwa kutumia rasilimali zilizopo kwa uwazi na uwajibikaji. LIWOPAC inafanya tafiti mbalimbali juu ya masuala yanayohusiana na programu zinazotekelezwa.

2.0 USHIRIKI WA WADAU

Katika utekelezaji wa shughuli kwa mwaka 2020, shirika limeweza kushirikiana na Serikali katika ngazi zote kuanzia ngazi ya kijiji, Kata, Wilaya hadi Mkoa. Pia ushirikiano na jamii umekuwa wa mafunzo kwa pande zote mbili. LIWOPAC inaendelea kufanya kazi kwa ushirikiano na wadau mbali mbali na Asasi za kiraia zenye mlengo unaofanana kama vile LSF, OXFAM Tanzania, SATF, WLAC, PANITA na TLS. Pia LIWOPAC ni mwanachama wa mitandao mbalimbali ya Asasi zisizo za kiserikali kama vile TAPANET, LINGONET, LANGO and TANLAP ili kufanikisha malengo yake mbalimbali. Wadau wengine walioshirikiana na shirika kwa mwaka 2020 ni kama wafuatao:-

- Wizara ya Afya, Maendeleo ya jamii, Jinsia, Wazee na Watoto
- Wizara ya Katiba na Sheria
- Halmashauri 12 za wilaya za mkoa wa Lindi na Mtwara.
- Mashirika ya Wasaidizi wa kisheria ya mkoa wa Lindi na Mtwara.
- Watendaji wa Vijiji na Kata
- Dawati la Jinsia la Polisi
- Viongozi wa Dini
- Washauri na Wawezeshaji
- Mashirika yasiyo ya kiserikali ya mkoa wa Lindi kama vile LISAWA, PEMWA, ROWODO, SDA, HURUMA FOUNDATION, BAKAIDS
- Vyombo vya habari: Redio, Televisheni na Magazeti
- Wanufaika/Wanajamii kwa ujumla.

Uongozi wa shirika unatoa shukrani za dhati kwa wadau wote waliofanikisha utekelezaji wa shughuli kwa mwaka 2020.

3.0 MATOKEO YA SHUGHULI ZA MIRADI.

3.1. Tokeo na.1: Kuongezeka kwa Upatikanaji wa Huduma bora za Msaada wa Kisheria katika jamii husika kufikia mwaka 2020.

3.1.1: Mafanikio

Uwezeshwaji wa kisheria unaofanywa kwa jamii, umefanya utoaji wa huduma ya msaada wa kisheria kuwa ni haki ya msingi kwa jamii hizo. Jamii yenye uelewa wa haki za msingi za binadamu imeanza kuchukua hatua kudai haki zao katika mamlaka husika. Kazi ya kutoa msaada wa kisheria imesaidia LIWOPAC sio kupata uzoefu kwenye masuala ya haki za binadamu bali imewezesha shirika kupata ruzuku zinazosaidia masuala ya utawala kama vile kulipa pango la ofisi, kununua vifaa vya ofisi, kulipa mishahara ya wafanyakazi na huduma ya mawasiliano.

LIWOPAC imekuwa ikitekeleza mradi uitwao *Kuboresha huduma za msaada wa kisheria mkoa wa Lindi na Mtwara* unaofadhiliwa na LSF ambao ulikuwa na lengo la kuongeza wigo na upatikanaji wa huduma za msaada wa kisheria, kuongeza jamii yenye uelewa wa sheria na kuhakikisha uendelevu wa huduma za msaada wa kisheria zinazotolewa. Katika mwaka 2020, mradi umefanikiwa kuwafikia wanufaika **988 (Me 306, Ke 682)** katika mikoa yote ya Lindi na Mtwara. Mashauri yaliyoongoza kuripotiwa ni pamoja na migogoro ya ndoa, migogoro ya ardhi na matunzo ya watoto.

3.2 Tokeo na.2: Kuongeza uelewa wa sheria kwa wanajamii ya Lindi na Mtwara kufikia mwaka 2020.

3.2 1: Mafanikio

Utoaji wa elimu ya kisheria imekuwa ni lengo kuu la mradi ili kuongeza uelewa kwa wanajamii. Wasaidizi wa kisheria kwa kushirikiana na LIWOPAC wamefanya jitihada kubwa za kuwafikia watu wengi ili huduma ya msaada wa kisheria ijulikane kwa wanajamii mbalimbali. Hivyo kutokana na ushirikiano huo baina ya LIWOPAC, wasaidizi wa kisheria na wadau wengine wa utoaji wa haki jumla ya watu **528,296 (Me 249,422 Ke 278,874)** wameweza kufikiwa na kuwezeshwa juu ya elimu ya kisheria katika mikoa ya Lindi na Mtwara.

Elimu iliyokuwa inatolewa ilihusu sheria mbalimbali kama vile ya Ardhi, Madai, Mirathi, Ndoa, Matunzo ya watoto, Taratibu za mahakama n.k. Elimu hii hutolewa kupitia njia mbalimbali ambazo ni pamoja na kutembelea siku za kliniki za wakinamama hospitalini, kutembelea vikundi vya bodaboda, VICOBA, wajasiriamali n.k, kwenda kutoa elimu mashuleni ikiwemo shule za msingi na sekondari, kufanya mabonanza, kutembelea kaya, kupitia mikutano ya hadhara na kwa njia ya vyombo vya habari hususani redio.

3.2.2 Mchanganuo wa idadi ya watu waliofikiwa na mradi wa LSF 2019/2020

1. Takwimu za mwaka 2019						
Malengo ya idadi ya watu elimu ya kisheria 2019	Malengo ya idadi ya watu msaada wa kisheria 2019	Idadi ya watu waliofikiwa na elimu ya kisheria 2019		Idadi ya watu walifikiwa na msaada wa kisheria 2019		Jumla ya watu waliofikiwa 2019
100,000	500	ME 60,947	KE 72,545	ME 134	KE 428	134,054
2. Takwimu za mwaka 2020						
Malengo ya idadi ya watu elimu ya kisheria 2020	Malengo ya idadi ya watu msaada wa kisheria 2020	Idadi ya watu waliofikiwa na elimu ya kisheria 2020		Idadi ya watu walifikiwa na msaada wa kisheria 2020		Jumla ya watu waliofikiwa 2020
200,000	1000	ME 249,422	KE 278,874	ME 306	KE 682	529,284

3.3 Tokeo na.3: Kuongezeka kwa uelewa wa Haki za kijinsia katika maeneo ya utekelezaji.

Mafanikio

3.3.1 Kuongezeka kwa matumizi bora ya huduma ya msaada kwa wahanga wa matukio ya ukatili wa kijinsia katika jamii


Takwimu za mwaka 2020 zinaonesha kuwa, wahanga 45 walitumia mifumo rasmi ya kuripoti matukio ya ukatili wa kijinsia kama inavyoonyesha kwenye mpangilio ufuatao; wahanga 15 walitoa taarifa kupitia dawati la jinsia polisi wilaya, wahanga wanne (4) walitoa taarifa kupitia kwa Afisa mtendaji wa kata, Wahanga 5 walitoa taarifa kupitia kwa Afisa ustawi wa jamii wa Halmashauri, wahanga 6 walitumia ofisi za watendaji wa vijiji kutoa taarifa, wahanga 8 walitumia mabalozi wa kupinga vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto kutoa taarifa na wahanga 7 walipeleka taarifa LIWOPAC kama kituo cha kutoa msaada wa kisheria. Takwimu zinaonesha kuwa ukatili wa kingono, ubakaji na ukatili wa kimwili ndio matukio ambayo yamekua yakiripotiwa mara kwa mara katika vituo vya kupokea mashauri ya ukatili wa kijinsia.

3.3.2: Kuongezeka kwa mabadiliko ya mitazamo na mienendo chanya katika jamii.

Katika tokeo hili tumepima asilimia ya wanawake kwa wanaume ambao wamefanyiwa mahojiano kupitia dodoso na ambao wameguswa moja kwa moja na shughuli za kimradi ili kubadili mitazamo na mienendo yao katika jamii na uelewa mpana wa matokeo hasi na sababu zinazopelekea ukatili wa kijinsia. Takwimu zinaonesha kuwa wanawake 6 kati ya 12 waliohojiwa wana uelewa juu ya madhara yanayotokana na ukatili wa kijinsia katika maeneo yao na 50% ambayo ni sawa sawa na wanaume 5 kati ya 8 ambao wamehojiwa wana uelewa juu ya madhara ya matukio ya ukatili wa kijinsia.

3.3.3: Serikali za mitaa kuwa na uwezo wa kuzitafsiri na kuzifanyia kazi sera na sheria zinazohusu usawa wa kijinsia katika jamii husika.


Katika kupima mabadiliko kwenye tokea hii, tumeangalia idadi ya watumishi wa Serikali za mitaa ambao wameweza kuzitafsiri sera na sheria katika maeneo yao ya kazi zinazohusu na kutetea usawa wa kijinsia. Matokeo yanaonesha kuwa kuna ongezeko la 12% kutoka kwenye tafiti ya awali ya msingi kama inavyofafanuliwa hapa. Mtendaji wa kata 16%, Mtendaji wa kijiji 16%, Afisa maendeleo ya jamii/ustawi 12% na dawati la jinsia polisi 8%.



Pichani: Viongozi wa Serikali za mitaa wakijengewa uwezo wa kuzitafsiri sera na sheria za usawa wa kijinsia.

3.3.4: Kuongezeka kwa utoaji huduma bora na salama kwa wahanga wa matukio ya ukatili wa kijinsia.

Takwimu zinaonesha kuwa na uboreshwaji wa huduma kwa 37%. Takwimu zinafafanua kuwa watendaji wa kata pamoja na wa vijiji wameingiza MTAKUWWA katika mipango kazi yao ya mwezi na robo mwaka. Mfano ofisi ya kata ya Kilolambwani waliandaa mpango kazi na kuanza kufuatilia kwa Mkurugenzi wa Manispaa Lindi kwa ajili ya kupata fedha za utekelezaji. Sambamba na ofisi ya kijiji cha Chilala waliweka ajenda katika ubao wa matangazo wa kijiji. Wahanga wa matukio ya ukatili wa kijinsia wamefafanua kuwa watoa huduma 3 kati ya 8 wamekuwa wakitoa huduma bora. Katika kuboresha huduma kwa wahanga wa ukatili wa kijinsia, mambo makuu yafuatayo wameyatajwa ambayo ni pamoja na watoa huduma wamekuwa na lugha nzuri, wanajali muda na kuongezeka kwa imani juu ya watoa huduma.



Pichani: Afisa mtendaji wa kijiji cha Rutamba na Mabalozi wakiandaa mpango kazi wa Kijiji katika vita dhidi ya ukatili wa kijinsia.

3.3.5: Kuongezeka kwa huduma zinazokidhi changamoto za wanawake waishio katika mazingira magumu katika jamii.

Matokeo yanaonesha kuwa wanawake 8 kati ya 12 waliofanyiwa mahojiano wameridhishwa na upatikanaji wa huduma kwa 66%. Takwimu pia zinaonesha kuwa watoa huduma wameweza kuwajali, kuwahudumia kwa lugha nzuri na kuwahudumia haraka sawa na kujali muda ambapo vyote hivi vimeweza kuongeza uaminifu baina ya wahanga wa matukio ya ukatili wa kijinsia pamoja na watoa huduma. Mbali na sababu tajwa hapo juu lakini vile vile mkazi mmoja alijitokeza na kutaka kuandikiwa WOSIA ili kuepuka changamoto zitakazotokea baadaye kwa mke na watoto baada ya kifo/vifo kutokea.

3.3.6: Kuongezeka kwa nafasi za wanawake katika uongozi.

Ngazi za kiutawala katika shirika la LIWOPAC inaonesha kuwa 50% ya wajumbe wa bodi ya shirika ni wanawake na 50% ni wanaume. Sambamba na ongezeko hili la kiungozi lakini pia sera ya usawa wa kijinsia imeandaliwa ambayo inafafanua usawa wa kijinsia katika nafasi mbalimbali za shirika na uongozi wa kidemokrasia ambao unajali haki ya mwanamke. Sera imeeleza kuwa haki za mwanamke zitalindwa ikiwa ni pamoja na kuthaminiwa kwenye nafasi ya ujumbe wa bodi ya shirika na masuala ya ajira katika shirika.

3.4 Tokeo na 4: Kuimarika kwa uelewa wa haki za mtoto.

3.4.1: Mafanikio

Shirika la LIWOPAC kupitia ufadhili wa shirika la SATF limefanikiwa kutoa msaada wa kuwasomesha watoto waishio katika mazingira magumu kwa ngazi mbalimbali za elimu kuanzia Elimu ya Msingi, Sekondari, Vyuo vya Ufundi, Vyuo vya Kati na Chuo kikuu. Watoto hao ni kutoka Wilaya 3 za Nachingwea, Lindi Manispaa na Mtama katika shule ya Wasichana Nachingwea, Farm 17, Misufini, Nyengedi, Mingoyo na Chikonji sekondari. Katika mwaka 2020 shirika limeweza kusajili watoto wapya 40 kutoka katika Wilaya tajwa hapo juu na kufanya jumla ya watoto 81. Aidha tumefanikiwa kuwasaidia watoto hao Bima ya afya, sare za shule, viatu, daftari, taa za sola, begi, taalo za kike, masweta, kalamu za wino, penseli, rula na mikebe.



Pichani: Afisa mradi wa mradi wa kusaidia watoto waishio katika mazingira magumu akiwapatia vifaa vya shule watoto katika manispaa ya Lindi.

3.5 Tokeo na. 5: Utafiti katika masuala yanayohusiana na utekelezaji wa programu za LIWOPAC umefanyika na taarifa kutolewa na kusambazwa kwenye maeneo husika.

3.5.1 Mafanikio:

Katika mwaka huu, LIWOPAC imefanya tathimini ya mwisho ya utekelezaji wa mradi wa kuboresha huduma za msaada wa kisheria katika mkoa wa Lindi na Mtwara. Tathimini hii ilifanyika kwa lengo la kuangalia ni kwa namna gani mradi umefanikiwa kufikia malengo

yaliyotarajiwa. Matokeo ya tathimini hiyo yatasaidia kutoa taarifa muhimu kwa LIWOPAC ambayo itawezesha kufikiria na kupanga kwa makini shughuli za utekelezaji kwa miradi ijayo. Pia tathimini hiyo ilikuwa na lengo la kupima ufanisi, ubora na uhalisia wa kutumia mfumo wa kuwa na shirika mlezi yaani (RMO-PU modal). Pia iliangalia matokeo ya mradi na uendelevu wa mradi hata mara baada ya kuisha.

Matokeo ya tathimini yanaonesha;

1. Ongezeko la uwezo wa kiutendaji kazi kwa LIWOPAC na wasaidizi wa kisheria.
2. Kuimarika kwa uelewa wa sheria kwa LIWOPAC na wasaidizi wa kisheria kwa mfano uelewa kwenye usuluhishi wa migogoro ya ardhi, migogoro ya ndoa, mirathi, matunzo ya watoto, madai, ukatili wa kijinsia na migogoro ya kazi.
3. Kuongeza kwa mtandao wa ushirikiano kwa LIWOPAC na wasaidizi wa kisheria. Kwa mfano LIWOPAC ina mtandao na mashirika walezi wa wasaidizi wa kisheria Tanzania nzima, mashirika ya wasaidizi wa kisheria wa Lindi na Mtwara. Pia mtandao na mashirika makubwa ya ndani na nje ya nchi.
4. Kuimarika kwa kitengo cha ufuatiliaji wa shughuli na matokeo ya miradi kwa LIWOPAC na wasaidizi wa kisheria.

Aidha LIWOPAC ndani ya mwaka 2020 imetoa matokeo ya tafiti nyingine ambayo nakala yake imeshatolewa. Tafiti hii imefafanua juu umuhimu na mchango wa mabalozi wa kupinga vitendo vya ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto katika jamii. Taarifa ya tafiti hii pia imefafanua juu ya changamoto ambazo wanakutana nazo mabalozi hawa katika utekelezaji wa majukumu yao ya kuripoti na kushughulikia matukio ya ukatili wa kijinsia.

4.0: MAFUNZO, CHANGAMOTO NA MAPENDEKEZO.

4.1 MAFUNZO

1. Utoaji wa elimu ya kisheria kupitia redio umeongeza wigo wa wasaidizi wa kisheria kujulikana wanafanya nini katika jamii waliopo ukilinganisha na hali ilivyokuwa hapo mwanzo. Eneo kubwa linalosikikika redio Mashujaa Fm, Safari Fm and Newala Fm radio imeongeza nafasi kwa watu wengi hususani wanawake kuelewa umuhimu wa wasaidizi wa kisheria katika jamii. Hivyo wanawake wanapata haki zao kupitia wasaidizi wa kisheria waliopo maeneo yao wanaojitangaza kwa kutumia vyombo vya habari.
2. Ushirikiano mzuri kati ya Wasaidizi wa kisheria na wadau wengine imepelekea kuongezeka kwa kuaminika kwa jamii. Jamii inakubaliana na kazi za wasaidizi wa kisheria kwa kuamua kwenda kupata msaada kwa wasaidizi wa kisheria. Kwa mfano Halmasahuri ya wilaya ya Nanyumbu, Mtama, Mtwara Mikindani, Liwale na Kilwa

wanapokea rufaa nyingi kutoka mamlaka za Serikali ili kuwasaidia watu kusuluhisha migogoro ya kisheria.

3. Uwekaji wa msaidizi wa kisheria kila kata kumesaidia kuongezeka kwa wanufaika wa msaada wa kisheria. Kufanya hivi kumeongeza upatikanaji wa huduma za msaada wa kisheria kwa karibu kwa wanajamii. Pia imeongeza uhusiano mzuri kati ya wanajamii na wasaidizi wa kisheria.

4.2 CHANGAMOTO

1. Msimu wa uchaguzi mkuu uliathiri shughuli za utoaji wa elimu ya kisheria kwa wanajamii. Hii ilipelekewa na wasaidizi wa kisheria kuomba vibali vya kwenda kutoa elimu lakini hawakupewa kutokana na kuhofiwa wataenda kufanya kampeni za kisiasa. Hivyo shughuli ya mikutano ya hadhara, mabonanza ikisimama kwa muda.
2. Pesa za nauli walizokuwa wanapewa wasaidizi wa kisheria zilikuwa hazitoshi kuwafikisha maeneo ya mbali ambayo jamii ilikuwa inawahitaji. Hii ilipelekea hata wakati mwingine kutumia pesa zao binafsi kufanya nauli kwenda kuwasaidia wanajamii.
3. Mlipuko wa ugonjwa wa Virusi vya Corona yaani COVID – 19 ulikwamisha baadhi ya shughuli ambazo zilikuwa kwenye mpango kazi kukamilika. Hii ni kwa wasaidizi wa kisheria na mabalozi wa kupinga ukatili wa kijinsia kutokana na kuzuiliwa kwa mikusanyiko katika jamii. Hivyo LIWOPAC iliwahamasisha kutumia njia nyingine mbadala ili kuwafikiwa watu kama vile njia ya utoaji elimu nyumba kwa nyumba kwa kuhakikisha wanavaa barakoa na kuzingatia umbali kati ya mtu na mtu.

4.3 MAPENDEKEZO

1. Serikali kwa kushirikiana na wadau na mashirika mbalimbali kama vile LSF iongeze idadi ya wasaidizi wa kisheria kufikia ngazi ya kijiji. Hii itaongeza upatikanaji wa huduma za msaada wa kisheria kwa karibu zaidi na wanajamii.
2. Pamoja na kuwa kazi ya usaidizi wa kisheria ni ya kujitolea, LIWOPAC tunawaomba LSF na wadau wengine kuongeza motisha kwa wasaidizi wa kisheria kwa kuwapatia posho ndogo ndogo. Kwa kufanya hivyo itasaidia kupunguza idadi ya wasaidizi wa kisheria wanaoacha kazi kutokana na kwenda kufanya shughuli nyingine za kiuchumi.
3. Wasaidizi wa kisheria kuanzisha shughuli mbalimbali za kutunisha mfuko wa mashirika yao. Hii itasaidia huduma kuendelea kutolewa kwa jamii pia kuimarisha hali za kiuchumi za wasaidizi wa kisheria wenyewe.
4. Kutokana na kutokuwa na uwiano sawa kati ya viongozi wanawake na wanaume katika Serikali za mitaa, tunaomba Serikali izingatie usawa wa kijinsia wakati wa utoaji

wa ajira kwa viongozi hao hususani maeneo ya vijijini kwa kuzingatia uwezo wa kila mmoja.

5.0. HITIMISHO NA VIAMBATANISHO

5.1. HITIMISHO

Shirika la LIWOPAC limefanya kazi kubwa katika utekelezaji wa shughuli ilizojipangia kwa mwaka wote wa 2020. Jitihada hizi zimeweza kusaidia makundi mbalimbali ya wanajamii katika mikoa ya Lindi na Mtwara. Jitihada hizi pia zimefungua fursa mpya katika uendeleu wa kupata huduma za kupinga vitendo vya ukatili wa kijinsia, huduma za msaada wa kisheria pamoja misaada ya watoto waishio katika mazingira magumu mkoani Lindi na maeneo ya jirani. Hata hivyo, ufanisi wa utekelezaji wa shughuli za miradi ni moja ya maandalizi ya shughuli zijazo zinazopaswa kutekelezwa na shirika. Uhusiano mzuri baina ya wafanyakazi na wanufaika umeleta chachu ya kujengeana uwezo, kubadilishana uzoefu na uelewa, maendeleo ya kitaalamu na ukaribu katika umilikaji wa rasilimali fedha.

5.2. VIAMBATANISHO

5.2.1: HABARI ZA MAFANIKIO

5.2.2: MPANGO KAZI WA MWAKA 2021

5.2.3: MAHESABU YA MWAKA YALIYOKAGULIWA

5.2.1.1: WASAIDIZI WA KISHERIA WAMSAIDIA MWANAMKE ALIYEACHIKA KUPATA MALI ZAKE.

Pili Luono (46), mkazi wa mtaa wa Mbae, manispaa ya Mtwara. Aliolewa na bwana Ahmad Nakuwa mwaka, 2002 nakupewa talaka mwaka 11/3/2017. Alisema katika ndoa yao walifanya mambo mengi ya maendeleo, ikiwa ni pamoja na kujenga nyumba na kununua shamba la mikorosho. Hata hivyo mume huyo alipooa mwanamke mwingine, mambo yalibadilika.

Alisema aliyekuwa mumewe alianza tabia ya kumdharau na kuacha kupokea ushauri. Muda wakukaa pamoja na kupanga mipango ya maendeleo ulikuwa haba. Lakini pia alifokewa na kupigwa pindi alipomuuliza sababu ya mabadiliko hayo yatabia ambayo yalikuwa na kila dalili ya kukwamisha mipango ya maendeleo yao.

Hali ilipokuwa mbaya Zaidi akaomba talaka jambo ambalo lilipokelewa vizuri na bwana Nakuwa kwasababu aliamini kwamba kwakuwa talaka imeombwa hivyo mke wake atakuwa amepoteza haki zake zote. Kwahiyo alimpa talaka na kumtaka aondoke kwenye nyumba yao.

Baada ya miezi mitatu, Pili alikwenda kuomba msaada katika kituo cha NERIO. Kwani katika kipindi chote cha miezi mitatu ya matazamio aliendelea kuishi kwenye nyumba hiyo baada ya kukaidi amri ya kuondoka. Msaidizi wa kisheria Bi Judith Chitanda alimuita bwana Nakuwa na kumuhoji kwanini alikuwa anamfukuza bila kumpa haki yake. Hata hivyo bwana huyo alisema asingeweza kuwasikiliza wasaidizi wa kisheria. Kwasababu walikuwa hawana mamlaka ya kumuhoji yeye ambae ni mtumishi wa serikali.

Hata hivyo msaidizi wa kisheria Judith Chitanda alimuonya kwamba akiendelea kuleta dharau wangemsaidia Pili kwenda kudai haki yake mahakamani. Kwani wasaidizi wa kisheria wapo kisheria na wanatakiwa kuheshimiwa. Baada ya kusikia hivyo alinywea na kuanza kumsikiliza," alisema Pili.

Alisema baada ya mabishano ya hoja kati ya Nakuwa na msaidizi huyo wa kisheria (Judith) , Nakuwa alikubali kukabidhi nyumba , vyombo vya ndani, samani na kipande cha shamba la mikorosho chenye mikorosho 30. Huku Nakuwa akiachiwa nyumba mbili na kipande cha mikorosho kilichobaki baada ya kumegewa Pili.

Kwa kauli yake mwenyewe Bi Pili anasema "Sidhani kama ningepewa nyumba hii kama nisingepata msaada kutoka kituo cha msaada wa kisheria. Mume wangu baada ya kunipa talaka alinitaka niondoke. Nikakimbilia kuomba msaada kwa wasaidizi wa kisheria ambao walipambana na kusababisha niachiwe nyumba hii".

Hata hivyo Judith alifichua kwamba miongoni mwa watu wasumbufu kupokea elimu wanapoitwa na kituo hicho ili kutafuta suluhu ya migogoro ni watumishi wa serikali. Alisema baadhi yao licha ya kutenda vitendo vya ukatili wa kijinsia lakini wanajiona wapo sahihi.

Nae Ahmad Nakuwa alikiri kutokea mgogoro huo na alisema alikubali kuacha nyumba na mali nyingine kwa moyo safi. Nibaada ya kuzungumza na wasaidizi wa kisheria wa NERIO. Huku akiweka wazi kwamba hana kinyongo na Pili.

Mkuu wa idara ya maendeleo ya jamii wa halmashauri ya manispaa ya Mtwara, Juliana Manyama alikiri kwamba kituo hicho kimekuwa ni msaada mkubwa katika kusuluhisha na kutatua migogoro katika jamii. Akiweka wazi kwamba ndio msingi wa kuanzishwa kwa mashirika na vituo vya msaada wa kisheria.

Alisema kwakuzingatia ukweli kwamba vituo na mashirika ya msaada wa kisheria na haki za binadamu yanamchango mkubwa katika kusuluhisha migogoro, ndiyo sababu yanafanya kazi kwa mujibu wa sheria. Yapo kisheia, yanatambulika na yamesajiliwa kwa mujibu wa sheria za nchi.

Bi Pili alisema wakati anapewa nyumba hiyo haikuwa na milango wala madirisha. Lakini ameweka milango na madirisha imara ya chuma. Pia ameongeza chumba kimoja na sebule kupitia fedha za faida ya mauzo ya biashara yake ya sabuni ambazo anatengeneza mwenyewe.

Chitanda ambae pia ni Afisa ufuatiliaji na tathimini wa NERIO alisema shirika hilo linatamani kila anayesaidiwa anaonesha mabadiliko ya kimaendeleo. Kwani ni dhahiri juhudi za shirika zitakuwa zimezaa matunda. Kwa kuzingatia hilo wanawatembelea ili kuwapa ushauri na kuwatia moyo.

5.2.1.2: KANISA KATOLIKI LAWASHUKURU WASAIDIZI WA KISHERIA KUMALIZA MGOGORO KWA AMANI

Kanisa katoliki parokia ya Makanya limewashukuru wasaidizi wa kisheria wa shirika la Community Harmony Prosperity Organization (CHPO) la wilayani Nanyumbu kwa kusuluhisha mgogoro wa ardhi baina ya kanisa hilo na baadhi ya wananchi wa kijiji cha Makanya, wilaya ya Nanyumbu mkoa wa Mtwara.

Shukrani hizo zilitolewa kijijini Makanya na padre Jacob Mchopa, alipozungumzia mgogoro mkubwa baina ya kanisa na baadhi ya wananchi waliojenga nyumba za makazi katika eneo la kanisa. Kwani ulifikia hatua ya kufikishwa mahakamani na baadhi ya wananchi hao. Alisema pamoja na mgogoro huo kuwa mkubwa, wasaidizi wa kisheria wa CHPO wameweza kusuluhisha na kumaliza kwa amani.

"Ninawashukuru sana, eneo lililochukuliwa ni mali ya kanisa lina hati ya umiliki kwa muda wa miaka 99, toka mwaka 1959. Lakini baadhi ya watu wamejenga, tulipowaambia waondoke walikataa katakata wakidai waliuziwa na mmoja wa watumishi wa parokia ya Makanya. Lakini wasaidizi wa kisheria walitukutanisha, nashukuru sana. Kwani tayari tumeelewana," alisema Paroko Mchopa.


Aliyataja makubaliano yaliyoafikiwa na pande zote ni kanisa kuwarejeshea fedha zao. Kila mmoja kiasi cha fedha alizonunulia. Huku akitoa wito kwamba kila anayehitaji kuongezewa muda wa kuishi katika eneo ambalo ametakiwa kuhama atume barua ya kuomba kuongezewa muda na apeleke kwa kanisa hilo. " Sisi kanisa tunahubiri upendo na amani, ndio maana tumekubali kuwarejeshea fedha zao ingawa waliuziwa na mtu na sio kanisa. Kwasasa tumekubaliana hadi mwakani, tarehe 20, Januari waachie maeneo hayo. Kama kuna

anayetaka kungezwa muda alete barua kwetu na aoneshe anaomba kuendelea kuishi kwa muda gani," alisema Mchopa.

Kuhusu mahusiano na jamii baada yakusuluhishwa alisema mahusiano ni mazuri sana wananchi wanashirikiana naye binafsi na kanisa. Akiweka wazi kwamba hata walioanza kuachia maeneo hawaoneshi kinyongo wala chuki. Mmoja wa wanaotakiwa kuachia eneo alilojenga, Omari Hausi alisema wamepokea uamuzi uliotolewa tarehe 20.9.2019 katani Nangomba ambao ulilenga kusuluhisha mgogoro huo. Huku akisema maeneo hayo waliuziwa na kamati ya halmashauri ya walei ya parokia ya Makanya. " Kwenye kikao kile tulibaini eneo hili ni mali ya jimbo na siyo kamati iliyotuuzia. Hata hivyo kanisa limekubali kuturejeshea fedha zetu na linafikiria kutuongozea muda wa kuishi, ni jambo jema tunashukuru," alisema Hausi.

Nae mkurugenzi wa CHPO, Michael Mkumba alisema wananchi wilayani Nanyumbu wameanza kujua umuhimu wa kituo hicho. Watu wengi wameanza kwenda kuomba ushauri kwenye kituo hicho badala ya kukimbilia mahakamani. Maelezo ambayo yaliungwa mkono na katibu tawala wa wilaya hiyo (DAS), Salum Palango ambae ofisi yake ipo bega kwa bega na shirika hilo. Akiweka wazi kwamba limesaidia kusuluhisha na kupunguza migogoro katika wilaya ya Nanyumbu.

BARUA ZA SHUKRANI



Katibu Mkuu,
Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto,
Chuo kikuu cha Dodoma, Kitivo cha Sanaa na Sayansi ya Jamii,
S.L.P 574,
40478, Dodoma Tanzania.

Nakala Kwa:

Katibu Tawala Mkoa wa Lindi,
S.L.P 1054,
Lindi.

Mkuu wa Wilaya ya Lindi,
S.L.P 1020,
Lindi.

Mkurugenzi Manispaa ya Lindi,
S.L.P 1070,
Lindi.

Mkurugenzi Mtendaji (W) ya Lindi,
S.L.P 328,
Lindi.

Mkurugenzi Mtendaji (W) ya Kilwa,
S.L.P 160,
Kilwa.

Mkurugenzi Mtendaji (W) ya Nachingwea,
S.L.P 291,
Nachingwea.

Mkurugenzi Mtendaji (W) ya Ruangwa,
S.L.P 01,
Ruangwa.

Mkurugenzi Mtendaji (W) ya Liwale,
S.L.P 05,
Liwale.

Afisa Maendeleo ya Jamii Mkoa,
S.L.P 1054,
Lindi.

Afisa Maendeleo ya Jamii (W) ya Lindi,
S.L.P 328,
Lindi.

Afisa Maendeleo ya Jamii Manispaa ya Lindi,
S.L.P 1070,
Lindi.

Polisi-Dawati la Jinsia Mkoa,
S.L.P
Lindi.

Polisi-Dawati la Jinsia (W) ya Lindi,
S.L.P
Lindi.

TAPANET,
S.L.P 6584,
Morogoro.

TANLAP,
S.L.P
Dar Es Salaam.

WLAC,
S.L.P 79212,
Dar es Salaam.

LINGONET,
S.L.P 92,
Lindi.

Hakimu Mkazi,
S.L.P 1062,
Lindi.

Mahakama ya Mwanzo,
S.L.P
Lindi.

LANGO,
S.L.P 554,
Lindi.

TLS Kanda ya Kusini,
S.L.P 1481,
Mtwara.

**LINDI WOMEN PARALEGAL AID CENTRE
(LIWOPAC)**

**ANNUAL REPORT AND AUDITED FINANCIAL STATEMENTS
FOR THE YEAR ENDED 31 DECEMBER 2020**

LINDI WOMEN PARALEGAL AID CENTRE

**ANNUAL REPORT AND AUDITED FINANCIAL STATEMENTS
FOR THE YEAR ENDED 31 DECEMBER 2020**

<u>TABLE OF CONTENTS</u>	<u>PAGE</u>
Abbreviations	iii
The Organization's information	iv
Directors' report	1 – 6
Statement of directors' responsibilities	7
Declaration of the head of finance	8
Report of the independent auditor	9 – 11
<i>Financial statements:</i>	
Statement of income and expenditure and other comprehensive income	12
Statement of financial position	13
Statement of changes in accumulated fund	14
Statement of cash flows	15
Notes to the financial statements	16– 27

LINDI WOMEN PARALEGAL AID CENTRE

ANNUAL REPORT AND AUDITED FINANCIAL STATEMENTS FOR THE YEAR ENDED 31 DECEMBER 2020

LIST OF ABBREVIATIONS

CPA – PP	Certified Public Accountant in Public Practices
ED	Executive Director
GAAP	General Accepted Accounting Principles
GBV	Gender Based Violence
IAS	International Accounting Standards
IESBA	International Ethics Standards Board of Accountants
ISA	International Standards on Auditing
LIWOPAC	Lindi Women Paralegal Aid Centre
LSF	Legal Services Facility
NBAA	National Board of Accountants and Auditors
NGO	Non-Governmental Organisation
NSSF	National Social Security Fund
PU	Paralegal Unit
RMOs	Regional Mentor Organization
SDL	Skills Development Levy
SMEs	Small and Medium Enterprises
TFRS	Tanzania Financial Reporting Standards
TZS	Tanzanian Shillings
USD	United States Dollars
WCF	Workers Compensation Fund
WHT	Withholding Tax

LINDI WOMEN PARALEGAL AID CENTRE

ANNUAL REPORT AND AUDITED FINANCIAL STATEMENTS FOR THE YEAR ENDED 31 DECEMBER 2020

THE ORGANIZATION'S INFORMATION

Registered office	Lindi Women Paralegal Aid Centre Jamhuri Street old CRDB Building, Lindi Municipal, P O Box 408, Lindi, Tanzania.
Principal bankers	CRDB Bank Plc Lindi Branch, P.O. Box, 266 Lindi, Tanzania.
Auditors	KPGL Audit Tax & Business Consultants Plot No. 25 Nyerere Road, Quality Centre Mall PO Box 4869, Dar es Salaam Email: info@kpgl.co.tz Web: www.kpgl.co.tz

LINDI WOMEN PARALEGAL AID CENTRE

DIRECTORS' REPORT FOR THE YEAR ENDED 31 DECEMBER 2020

1 INTRODUCTION

The Directors of LINDI WOMEN PARALEGAL AID CENTRE are pleased to submit their report together with the audited financial statements for the year ended 31 December 2020, which disclose the state of affairs of Lindi Women Paralegal Aid Centre as at that date. This Director's report has been prepared in accordance with the Tanzania Financial Reporting Standards (TFRS) No. 1, Director's Report issued by National Board of Accountants and Auditors (NBAA).

2 INCORPORATION

